Jarida la DCEA
TOLEO LA NNE 2025/2026
ISSN NO. 978 - 9912 - 9896 - 1 - 0

# DAWA ZA KULEVYA

Kataa Dawa za Kulevya, Timiza Malengo Yako

HALIUZWI











**KUDHIBITI Upatikanaji wa Dawa za Kulevya**

**Kupunguza UHITAJI wa Dawa za Kulevya**

**Kupunguza MADHARA ya Matumizi ya Dawa za Kulevya**

**Kuimarisha USHIRIKIANO wa Kikanda na Kimataifa Kudhibiti Dawa za Kulevya**













## Yaliyomo


Uhalalishaji wa Bangi: Fursa au Hatari kwa Jamii?



Uk.3&4


Sheria Inasemaje Kuhusu Kuwalinda Wasiri



Uk.5

Dawa Mpya za Kulevya Tishio Jipya Duniani

Uk.6&7





Matukio Pichani >>>

Uk.10&11

Serikali ya Awamu ya Sita Yavunja Rekodi Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya



Uk.12&13

Dcea Yatunukiwa Tuzo ya Uandaaji Bora wa Taarifa za Fedha kwa Mashirika ya Umma



Uk.16

Katuni >>>

Uk.21&22

Tahariri

# Tiba ya Uraibu wa NPS Bado ni Changamoto, Tushirikiane Katika Mapambano

*KATIKA miaka ya hivi karibuni, dunia imekubwa na changamoto ya ongezeko la kasi la dawa mpya za kulevya, zinazojulikana kama New Psychoactive Substances (NPS).*

*Dawa hizi hutengenezwa kwa kuiga vichocheo vya dawa za kulevya zinazofahamika na kudhibitiwa kimataifa kama vile bangi, heroin, mirungi, cocaine, methamphetamine na dawa nyingine.*

*Uzalishaji wake hufanyika kwa siri katika maeneo mbalimbali, ikiwemo maabara bubu, kwa kutumia kemikali bashirifu au mimea, kisha husambazwa kwa njia zisizo rasmi katika maeneo mbalimbali duniani.*

*Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC), hadi Mei 2025, dawa mpya zakulevya zilifikia aina 1,341 kote duniani, idadi inayoonyesha ukubwa wa tatizo. Wahalifu wa dawa hizi za kulevya kutumia mbinu za kisasa na teknolojia ya hali ya juu, kuzisambaza kwa kasi, kupitia njia mbalimbali ikiwemo mitandao ya kijamii ya siri (dark web). Hali hii inaongeza ukubwa wa tishio kwa afya ya jamii na mustakabali wa kizazi kijacho.*



*Matumizi ya dawa za kulevya aina ya NPS yana athari kubwa kiafya ikiwa ni pamoja na kusababisha matatizo ya akili kwa haraka, kupoteza kumbukumbu na hata vifo vya ghafla. Aidha, tiba ya uraibu wa NPS bado ni changamoto kubwa kutokana na mabadiliko ya mara kwa mara ya muundo wa dawa hizo.*

*Ulinzi wa jamii yetu dhidi ya tatizo la dawa za kulevya ni jukumu letu sote. Pamoja na Serikali ni wajibu wa kila mzazi, mlezi, mwalimu wanasiasa kiongozi wa dini na wakimila, kutumie kila fursa kuelimisha vijana kuhusu hatari hii, kuwajengea uwezo wa kusema hapana kwa vishawishi, na kuwashirikisha katika shughuli chanya zinazowajenga kimaadili na kifikra.*


*Zaidi ya hayo, familia zinapaswa kujenga mawasiliano ya wazi na watoto wao, kufuatilia mwenendo wa kila siku wa vijana, na kuchukua hatua mapema wanapoona mabadiliko ya tabia yanayoashiria hatari.*

*Pia, jamii inapaswa kulinda maadili yetu kwa kukuza misingi ya kidini, uzalendo na nidhamu shirikishi.*

*Kwa pamoja, tukisimama kidete wazazi, walimu, viongozi wa dini, serikali na mashirika ya kiraia tunaweza kuwahepusha vijana wetu dhidi ya uharibifu huu wa kimfumo unaosababishwa na dawa mpya za kulevya. Huu ni wakati wa kuchukua hatua. Ustawi wa taifa letu unategemea afya bora, fikra na tabia njema za vijana wa leo.*

*Aretas Lyimo*
***Kamishna Jenerali***

Picha ya Jarida




**Jarida hili limeandaliwa na**
Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

**BODI YA WAHARIRI**

**Mwenyekiti**
*Aretas J. Lyimo*
***Kamishna Jenerali***

**Katibu**
*Florence B. Khambi*
***Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano***

**Wajumbe**
*Dkt. Peter P. Mfisi*
*Salmin K. Shelimoh*
*Moza K. Makumbuli*
*Ziliwa P. Machibya*
*Christina G. Rweshabura*
*Upendo K. Chenya*
*Daniel M. Kasokola*
*Lilian B. Matho*
*Seleman M. Edward*

**SHUKRANI**

*Haji Abeid*
***Msanifu na Mchora Katuni***

# *Jamii Ikiamua Tatizo la Dawa za Kulevya Litabaki Historia*

*PAMOJA na nia thabiti ya Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha jamii inakuwa huru bila biashara wala matumizi ya dawa za kulevya, bado jukumu kubwa linabaki kwa mwananchi kushiriki kikamilifu kwenye mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya.*

*Matumizi na biashara ya dawa za kulevya yana madhara mkubwa kiafya, kiuchumi, kijamii na pia ni tishio kwa usalama wa Nchi yetu. Athari hizi zinamgusa mtu mmoja, familia na jamii kwa ujumla hivyo kuharibu ustawi wa Taifa letu.*

*Kutoa taarifia kwa Mamlaka kuhusu uhalifiu wa dawa za kulevya unaofianyika katika maeneo yetu tunayoshi ni nyenzo muhimu katika kuhakisha dawa za kulevya hazizalishwi, haziingizwi na wala hazisambazwi katika jamii.*

*Jamii inahimizwa kutowanyanyapaa waraibu wa dawa za kulevya, badala yake wawasaidie kwenda kwenye vituo vya tiba ya uraibu wa dawa za kulevya pamoja na nyumba za upataji nafiuu zilizopo nchini. Waraibu waliopo kwenye hatua za uponyaji pia wasinyanyapaliwe bali wasaidiwe zaidi ili waweze kujitegemea kiuchumi na kurejea kwenye jamii na kushiriki katika ujenzi wa taifa.*

*Tanzania huru bila dawa za kulevya inaanza na Mwananchi mwenyewe kwa kutotumia dawa za kulevya na Kutoa taaarifia za uhalifiu wowote unaofianyika kuhusu dawa za kulevya kwenye maeneo yao. Ushiriki wa mwananchi katika jamii kwenye mapambano dhidi ya dawa za kulevya ni nyenzo muhimu katika kuendeleza jitihada za maendeleo zinazofianywa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.*



*Florence Khambi*
***Mhariri***



**NAMBA YA MAWASILIANO BILA MALIPO**

**119**

Sisi ni Nani?

# Ifahamu Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) ni Taasisi ya Serikali iliyoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Mamlaka hii ilianzishwa kwa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya Mwaka 2015 na kuanza kufanya kazi rasmi mwezi Februari, 2017.

## Majukumu ya Mamlaka:

Majukumu ya Mamlaka kama yalivyoainishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria Namba 5 ya mwaka 2015, ni kufafanua, kuhamasisha udhibiti wa dawa za kulevya, kuratibu na kutekeleza hatua zote zinazoelekezwa katika udhibiti wa dawa za kulevya.

Katika kutekeleza majukumu hayo Mamlaka inafanya kazi zifuatazo:

i. Kusimamia utekelezaji wa mikataba ya kimataifa, maazimio na makubaliano katika kudhibiti dawa za kulevya;

ii. Kuandaa na kutekeleza mpango wa Taifa wa kudhibiti dawa za kulevya;

iii. Kutengeneza miongozo inayoelezea tatizo la dawa za kulevya na madhara yake katika jamii;

iv. Kuboresha na kurekebisha sheria na kanuni za udhibiti wa dawa za kulevya;

v. Kuhamasisha udhibiti wa matumizi na biashara ya dawa za kulevya ikiwemo kutoa elimu juu ya madhara ya dawa za kulevya, kusambaza taarifa kwa umma na juhudi nyingine za udhibiti;

vi. Kuchukua hatua stahiki za kupambana na biashara ya dawa za kulevya zikiwemo kukamata, kupekua na kufanya uchunguzi wa masuala yanayohusiana na dawa za kulevya;

vii. Kuzuia, kupeleleza na kuchunguza uchepushwaji wa dawa za tiba zenye madhara ya kulevya pamoja na kemikali zilizosajiliwa kutoka kwenye vyanzo halali wakati huo huo kuhakikisha dawa hizo zinapatikana kwa matumizi ya tiba, biashara na mahitaji ya kisayansi;

viii. Kuanzisha mfumo thabiti wa ukusanyaji taarifa na uchambuzi katika ngazi ya Taifa kuhusu matumizi na biashara ya dawa za kulevya;

ix. Kuhamasisha, kuratibu na kuhakikisha jitihada za ushirikiano wa kimataifa katika kudhibiti wa dawa za kulevya zinaimarishwa;

x. Kufanya, kuwezesha na kuratibu tafiti zinazohusiana na dawa za kulevya;

xi. Kuratibu na kuwezesha wadau wanaojihusisha na udhibiti wa matumizi na biashara ya dawa za kulevya;

xii. Kuelimisha na kuhamasisha jamii kushiriki katika mapambano dhidi ya matumizi na biashara ya dawa za kulevya;

xiii. Kutoa mafunzo kwa watendaji wanaojihusisha na udhibiti wa matumizi na biashara ya dawa za kulevya, fedha haramu na kemikali bashirifu;

xiv. Kufanya uchunguzi wa sayansi jinai.

## Misingi Muhimu:

### Uadilifu

Kuzingatia kanuni za uadilifu na ukweli ili kutenda haki bila upendeleo.

### Ushirikiano

Kuimarisha ushirikiano na wadau pamoja na jumuiya ya kimataifa katika jitihada za kupambana na kudhibiti dawa za kulevya.

### Uwajibikaji

Kufanya kazi kwa kuzingatia maslahi ya umma ili kuilinda jamii dhidi ya matumizi, biashara na madhara ya dawa za kulevya.

### Ubunifu

Matumizi ya njia/mbinu bora zaidi zinazokidhi kutatua changamoto mpya katika udhibiti wa dawa za kulevya.

### Weledi

Kuwa na timu ya wataalamu wanaofanya kazi kwa weledi na maarifa.

### Usiri

Kuweka siri ya vyanzo vya taarifa za dawa za kulevya ili kuwalinda watoa taarifa.

### Ufanisi

Kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili kutimiza malengo.

Katika kutekeleza majukumu hayo, Mamlaka inashirikiana na Taasisi nyingine za Kitaifa na Kimataifa, Asasi za kiraia, Vyombo vya habari na jamii kwa ujumla.

Mjadala



*WANANCHI wa wilaya ya Tarime wakishiriki katika uteketekezaji wa mashamba ya bangi kuunga mkono juhudi za Serikali katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.*

# Uhalalishaji wa Bangi: *Fursa au Hatari kwa Jamii?*

**Na Lilian Matho**

BANGI ni aina ya dawa ya kulevya inayotokana na mmea unaoitwa *"Cannabis"*. Mmea huu una jamii nne, ambazo ni *sativa, indica, ruderalis na hybrid.* Kati ya hizo, bangi inayotumika zaidi kwa ajili ya kustarehesha na kusababisha madhara kwa watumiaji ni *Cannabis Sativa na hybrid.*

Matumizi ya bangi yameendelea kukithiri kwa wingi hapa nchini na Duniani kwa ujumla. Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya mwaka 2024, inayo andaliwa na Shirika la kumataifa linaloshughulikia dawa za kulevya na Uhalifu **(UNODC),** inakadiriwa kuwa takribani watu milioni 228 wenye umri kati ya miaka 15 - 64 walitumia bangi Duniani mwaka 2022.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, asilimia 70 ya watumiaji wa bangi ni wanaume na asilimia 30 ni wanawake. Matumizi ya bangi ni moja ya chanzo cha matumizi ya dawa za kulevya za viwandani kama vile heroin, cocaine. Aidha, takribani watoto milioni 13.5 wenye umri wa kati ya ya miaka 15-16 walitumia bangi mwaka 2021. Matumizi ya bangi katika umri mdogo yanaweza kusababisha uharibifu mkubwa wa mfumo wa fahamu kwa kuwa ubongo wa watoto unaendelea kukua.

## Uhalalishaji wa bangi

Katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwepo na msukumo mkubwa wa kuhalalishwa matumizi ya bangi Kimataifa ikiwemo bara la Afrika. Madai ya msukumo huo uko zaidi kwenye uzalishaji, chazo cha mapato kwa taifa, tiba, na kujistarehesha.

Kwa nchi za Afrika ikiwemo Tanzania, msukumo huu ulichochewa zaidi na mkanganganyiko wa taarifa iliyotolewa na Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya Duniani *Commission on Narcotic Drugs* **(CND)** ya kuiondoa bangi kwenye jedwali la nne mwaka 2021. Dawa za kulevya aina ya Nakotiki zilitengwa kwenye majedwali *(scheldules)* manne kutokana na uwezo wa kusababisha uraibu na madhara kwa watumiaji.

***(N.B. Dawa za kulevya aina ya Nakotiki ni dawa zinazotokana na mimea.)***

Dawa ya kulevya aina ya bangi iliwekwa kwenye majedwali mawili. Jedwali la Kwanza (I): Linahusisha dawa za kulevya zenye uwezo mkubwa wa kusababisha uraibu kwa haraka na kuleta madhara makubwa kwa watumiaji. Baadhi ya dawa zingine zilizopo kwenye jedwali hilo ni heroini na cocaine. Pia iliwekwa katika Jedwali la Nne (IV) Linalohusisha dawa za kulevya zilizopo kwenye Jedwali la Kwanza, lakini zinaweza kutumika kutengenezea dawa za tiba.

Hata hivyo, faida inayopatikana kutokana na kutengenezea dawa za tiba ni ndogo kulinganisha na hasara inayotokana na madhara yake. Kutokana na Bangi kuwekwa katika majedwali hayo mawili, Nchi nyingi zilikuwa zinasita kuruhusu kilimo cha bangi kwa ajili ya kutengenezea dawa za tiba.

Shirika la afya Duniani **(WHO),** lilikusanya tafiti mbalimbali zilizofanyika juu ya bangi kutumika kutengenezea dawa za tiba. Baada ya kuzipitia tafiti hizo, lilijiridhisha kuwa, pamoja na madhara yanayosababishwa na bangi, Dunia inaweza kunufaika kutokana na matumizi ya bangi katika kutengenezea dawa za tiba.

Kutokana na matokeo hayo, Shirika la afya Duniani liliamua kupeleka maombi kwa Tume ya kudhibiti dawa za kulevya Duniani *Commission on Narcotic Drugs* ya kuiondoa bangi kwenye jedwali la nne, ili nchi zinazotaka kuruhusu kilimo cha bangi kwa ajili ya kutengenezea dawa za tiba ziruhusiwe.

Baada ya CND kupokea ombi la WHO juu ya kuiondoa bangi kwenye jedwali la nne, iliamua kulipeleka suala hilo kwenye kikao chake cha 63 ili suala hili liweze kupigiwa kura na wanachama wote. Kura hii ilipigwa tarehe 2 Desemba, 2020. Matokeo ya kura hiyo yalionesha kuwa, nchi 52 zilipiga kura, kati ya hizo, nchi 27 ziliridhia bangi kuondolewa katika jedwali la nne na nchi 25 zilikataa. Nchi moja (UKRAINE) haikupiga kura.

Kutokana na Matokeo hayo, Mwaka 2021 CND ilitangaza rasmi kuiondoa bangi kwenye jedwali la nne. Hata hivyo, Tume hiyo ilisisitiza kuwa, Bangi bado ni dawa hatari ya kulevya kwa afya ya jamii kwa kuwa bado ipo katika jedwali la kwanza na iendelee kudhibitiwa.

***N.B. Kuondolewa kwa bangi kwenye jedwali la nne haina maana kuwa CNB imehalalisha matumizi ya bangi duniani, hili lilifanywa ili nchi zinazotaka kuruhusu kilimo cha bangi kwa ajili ya kutengenezea dawa za tiba ziweze kufanya hivyo bila kusita. Bangi bado ni dawa ya kulevya inayoendelea***

*>>> Inaendelea Ukurasa wa 4*

# Uhalalishaji wa Bangi

<<< Inatoka Ukurasa wa 3

*kudhibitiwa duniani.*

## Nchi zilizohalalisha bangi

Kwa sasa, nchi **65** kati ya nchi 193 wanachama wa Umoja wa Mataifa zipo katika hatua mbalimbali za kuhalalisha kilimo, biashara na matumizi ya bangi. Hatua hii hutofautiana kati ya nchi na nchi kama ifuatavyo.

i. Nchi 9 zimehalalisha matumizi kwa ajili ya starehe na biashara *(legalization of cannabis)* ambapo bangi haidhibitiwi kisheria, na watu wanaweza kuruhusiwa kulima, kumiliki, kufanya biashara na kuitumia. Pia, udhibiti kwenye soko ni sawa na udhibiti wa pombe au tumbaku.

ii. Nchi **17** zimeondoa katazo la bangi la kijinai *(Decriminalization of Cannabis)*, hivyo, zimeruhusu kumiliki na kutumia bangi kwa kiwango kilichowekwa kisheria. Hata hivyo, sheria inaweka kipengele cha Polisi kuweza kukamata na kutaifisha dawa hizo kutoka kwa mtu anayekiuka taratibu zilizowekwa.

iii. Nchi **39** zimeruhusu kilimo cha bangi kwa ajili ya kutengenezea dawa za tiba viwandani na tafiti za kisayansi. Nchi hizo zimetengeneza Udhibiti *(Regulation)* kwa kuweka mifumo ya kisheria na kuweka vigezo vinavyoamua ni nini kiruhusiwe au kisiruhusiwe ili kuhakikisha kuwa bangi hiyo haitumiki kinyume cha makusudio. Mifumo hiyo inajumuisha udhibiti wa kilimo, biashara, umiliki na usambazaji.

Barani Afrika, nchi ambazo zimeruhusu bangi kwa namna moja au nyingine ni pamoja na Lesotho (tiba, biashara), Zimbabwe (tiba, tafiti na biashara), Afrika ya Kusini (matumizi binafsi, na starehe), Zambia (tiba, na kwa ajili ya uzalishaji viwandani), Malawi (biashara, uzalishaji viwandani na tiba), Rwanda (tiba na biashara), Morocco (tiba na uzalishaji viwandani), Ghana (tiba na uzalishaji viwandani), Uganda (tiba na uzalishaji viwandani), eSwatini (tiba na biashara).

## Sababu zinazotajwa kuruhusu uzalishaji wa bangi

- Kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato na kukuza uchumi kupitia viwanda kwa kuwa bangi jamii ya "Hemp" inahusishwa na uzalishaji wa malighafi za viwandani kama vile nyuzi za kushonea nguo, na vifaa vya ujenzi,
- Kudhibiti biashara haramu kwa kuifanya halali na hivyo, kuwaondolea nguvu wahalifu na kupunguza makosa ya jinai,
- Kudhibiti ubora wa dawa na bidhaa zinazotokana na bangi kwenye soko kwa kuweka viwango vya ubora vinavyokubalika,
- Kuzalisha ajira kutokana na fursa za biashara na uwekezaji,
- Kuzalisha dawa kwa ajili ya tiba kwakuwa bangi inahusishwa na tiba ya kuongeza amu ya kula, kuzuia maumivu, kutapika na kichefuchefu kwa wagonjwa wa kansa na HIV,
- kutumika kwenye imani za kidini na baadhi ya sherehe za kijadi.

Mwelekeo wa hivi sasa unabainisha kuwa, nchi zilizohalalisha biashara, kilimo na matumizi ya bangi zinakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo, kushindwa kudhibiti mazao ya bangi kwa malengo kusudiwa hivyo kusababisha ongezeko la matumizi ya dawa hiyo, ongezeko la magonjwa ya akili pamoja na ongezeko la vitendo vya uhalifu. Vilevile nchi hizo zinakabiliwa na ukosefu wa masoko ya bidhaa zitokanazo na bangi na hivyo kusababisha bangi iliyozalishwa kuchepushwa na kuuzwa katika masoko ya ndani na nje ikiwemo kuingizwa nchini Tanzania.

Halikadhalika, hakuna tafiti za kutosha *(clinical trials)* kuthibitisha ubora na madhara yatokanayo na matumizi ya dawa zenye viambata vya bangi jambo ambalo linaweza kuhatarisha usalama wa wagonjwa. Hata hivyo, tafiti mbalimbali zinabainisha athari zitokanazo na biashara na matumizi ya bangi ambayo ni pamoja na kiafya, ongezeko la matumizi ya dawa za kulevya na hasa kwa vijana ambao ni nguvu kazi.

Kimsingi kutokana na changamoto nyingi zilizoainishwa, nchi zilizohalalisha kilimo cha mazao ya bangi hazijafikia matarajio yaliyokusudiwa. Hivyo, inashauriwa kila nchi kuchukua tahadhari juu ya msukumo uliopo wa kuhalalisha biashara na matumizi ya bangi ili:

- Kuzuia athari za kiafya zinazoweza kujitokeza na hasa kwa vijana kutokana na matumizi ya bangi,
- Kuzuia kuongezeka kwa uhalifu na kulinda maadili kwa jamii yetu,
- Kuzuia gharama kubwa zinazoweza kujitokeza kwa ajili ya tiba na udhibiti,
- Kuzuia migogoro kati ya Wananchi wenye kipato kidogo na kampuni za kigeni (corporate capture) zitakazokuwa na uwezo wa kukidhi vigezo vya kupewa vibali, kwani bangi inayolimwa hapa nchini haikidhi vigezo vya kuweza kutengenezea dawa tiba.
- Kulinda usalama wa chakula kwa kuzuia matumizi ya ardhi kujikita kwenye kilimo cha bangi,
- Kuzuia uhalibifu wa vyanzo vya maji, ekolojia, ukataji wa misitu na hivyo kulinda mazingira,
- Kuzuia ongezeko la matumizi zaidi ya dawa za kulevya kwa kuwa bangi ni mojawapo ya dawa za kulevya zinazochochea matumizi ya dawa nyingine,
- Nchi ipate nafasi ya kufanya tafiti zaidi kubaini madhara au faida za biashara, na matumizi ya bangi.

Nchini Tanzania, kilimo, biashara, usafirishaji, na matumizi ya bangi ni kosa sheria. Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya mwaka 2015 inapiga marufuku shughuli zote zinazohusiana na bangi, isipokuwa kwa madhumuni maalum ya kisayansi na matibabu kwa kibali cha Mamlaka husika. Kutokana na sheria hii, mtu yeyote atakayejihusisha na kilimo, biashara, au matumizi ya bangi anaweza kuchukuliwa hatua kali za kisheria. Kifungu cha 11 (1) (b) na 15 (1) (a) cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kinabainisha adhabu hizo.

# Sheria Inasemaje Kuhusu Kuwalinda Wasiri

## *...Ilitungwa na Bunge Kuwalinda Wasiri ili Kuhakikisha Usalama Wao*

**Na Lilian Matho**

ULINZI wa wasiri ni msingi muhimu katika mapambano dhidi ya uhalifu wa fanyabisha wa dawa za kulevya. Bila ulinzi wa kutosha, watu wengi huogopa kutoa taarifa zinazohusiana na wafanyabiashara wa dawa za kulevya. hali inayoweza kuzuia na kuchelewesha ukamataji wa wafanyabiashara wa dawa za kulevya na hatimaye kukwamisha utekelezaji wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Bunge lilitunga Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya na kuweka vifungu vinavyohusiana na kuwalinda wasiri ili kuhakikisha usalama wao.

### DCEA ina jukumu gani katika kuwalinda wasiri?

Kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya [Sura 95], Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ina jukumu la kulinda siri za watoa taarifa kuhusu biashara ya dawa za kulevya, kufanyia kazi taarifa zote zinazopokelewa ili kuhakikisha wafanyabiashara ya dawa za kulevya wanachukuliwa hatua na kutoa motisha kwa watoa taarifa ambao taarifa zao zitafanikisha kukamatwa kwa wahalifu wa dawa za kulevya.

Aidha, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya chini ya kifungu cha 42(2) inakataza watu kutoa taarifa za uongo zinazoweza kusababisha kufanyika kwa ukamataji au upekuzi kwa kutoa adhabu ya faini isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo cha miezi sita au kutumikia adhabu mbili zote kwa pamoja. Sheria hii chini ya kifungu cha 47(2) imewapa nguvu watumishi wanaotekeleza Sheria hii kuwalinda wasiri wao kwa kutolazimishwa kusema mahali walipopata taarifa au vyanzo vyao vya taarifa kuhusiana na wafanyabiashara wad awa za kulevya.

Pia, Sheria kwa mujibu wa Kifungu cha







19(1) inawataka watu/jamii kutoa taarifa za dawa za kulevya endapo wataona eneo, boma, chombo cha usafirishaji wanachomiliki au kusimamia kinatumika kwa lengo la kutayarisha, kuvuta, kuuza kujidunga dawa za kulevya

### Mtu anawezaje kutoa taarifa kuhusu uhalifu wa dawa za kulevya?

Mtu yeyote anaweza kutoa taarifa kuhusuwafanyabiashara wa dawa za kulevya na mitandao yao kupitia njia mbalimbali, huku akihakikishiwa usiri na ulinzi wa taarifa zake. Taarifa hizo zinaweza kutolewa kupitia:

**Kupiga Simu** – Piga simu ya bure kupitia kituo cha huduma kwa wateja cha Mamlaka (Call Centre) kwa namba 119.

**Kutembelea ofisi za DCEA** – Taarifa zinaweza kutolewa moja kwa moja katika ofisi za DCEA zilizopo:

- **Makao Makuu – Kivukoni, Dar es Salaam.**
- **Kanda ya Ziwa – Kapripoint, Mwanza**
- **Kanda ya Kati– Itega, Dodoma**
- **Kanda ya Pwani – Shangani, nyumba za TBA, Mtwara**
- **Kanda ya Kaskazini – Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Arusha**
- **Kanda ya Nyanda za juu Kusini – Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Mbeya.**

Kadhalika, taarifa inaweza kutolewa kupitia barua pepe ya Mamlaka **info@dcea.go.tz**, Mitandao ya Kijamii – DCEA inapatikana kwenye:

**Facebook** @dceatanzania
**X** @dceatanzania
**Instagram** @dcea tanzania
**Youtube** DCEATV

na Threads kwa jina **@dceatanzania** na kupitia Tovuti Rasmi ya Mamlaka **www.dcea.go.tz** na kuwasilisha taarifa yako kwenye sehemu maalum.

Ulinzi wa wasiri ni jukumu la msingi katika kuhakikisha mitandao ya wafanyabiashara wa dawa za kulevya inakomeshwa. Ni dhahili kuwa, Mamlaka haiwezi kufanikisha jukumu hili peke yake bila kushirikiana na jamii. Kila mwananchi ana wajibu wa kushiriki katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya kwa kutoa taarifa za wahalifu wa dawa hizo kwani taarifa zinazotolewa zinaweza kuwa na mchango mkubwa katika kuokoa maisha ya vijana wa Tanzania dhidi ya janga la dawa za kulevya na mustakabali wa taifa kwa ujumla.

# Dawa Mpya za Kulevya Tishio Jipya Duniani



Na Seleman Edward

KATIKA miaka ya hivi karibuni, dunia inakabiliwa na ongezeko kubwa la dawa mpya za kulevya, zinazojulikana kama *New Psychoactive Substances (NPS)*. Dawa hizi hutengenezwa kwa kuiga vichocheo vya dawa za kulevya zinazodhibitiwa kimataifa kama vile bangi, heroin, mirungi, cocaine, methamphetamine na dawa nyingine. Uzalishaji wake unaweza kufanyika kwa siri sehemu yoyote ile ikiwemo kwenye maabara bubu kwa kutumia kemikali bashirifu au mimea na baadaye kusambazwa katika maeneo ya starehe, mikusanyiko ya watu,shuleni, vyuoni na maeneo mengine ya kufanana na hayo.

Uwepo kwa dawa mpya za kulevya, unatokana na udhibiti mkubwa unaofanywa na vyombo vya udhibiti pamoja na maendeleo ya sayansi na teknolojia yanayopelekea uzalishaji wa haraka wa kemikali ambapo baadhi ya waalifu hutumia mwanya huo kuzichepusha na kutengeneza dawa za kulevya.

Dawa hizi huongezeka kwa kasi kubwa kuliko udhibiti wake, hivyo kuweka tishio kubwa la kiafya na kiusalama katika nchi na dunia kwa ujumla. Kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Umoja wa Mataifa inayoshughulika na Dawa za Kulevya na uhalifu wa kupangwa (UNODC), hadi kufikia Desemba 2024 kulikuwa na jumla ya dawa mpya zipatazo **1,253** duniani. Miongoni mwa dawa mpya za kulevya zinazotengenezwa kutokana na kemikali bashirifu ni;

i. **Synthetic Cannabinoids (31.7%):** Ni dawa zinazofanana na bangi lakini zenye athari mara 100 zaidi.

ii. **Synthetic Cathinones (34.6%):** Vichangamshi vinavyofanana na mirungi ya viwandani na "Amphetamine Type Stimulants" mfano ni "MDVP",

iii. **Hallucinogens (15%):** Dawa zinazobadilisha hali ya ufahamu wa mtu na kuona mambo tofauti na uhalisia.

iv. **Synthetic Opioids (12%):** Ni dawa mpya za kulevya zenye sifa ya afyuni (12%) mfano ni dawa jamii za fentanili, nitazenes na piperazines. Dawa hizi zinaweza kusababisha kifo kwa dozi ndogo.

v. **Sedatives/Hypnotics (4%):** Ni dawa zinazoathiri na kupumbaza akili, kama benzodiazepines.

vi. **Dissociatives (3%):** Ni dawa zinazoathiri uwezo wa mtumiaji kujitambua, mfano phencyclidine (PCP).

## Madhara ya Dawa Mpya za Kulevya

Madhara ya dawa hizi ni makubwa ikilinganishwa na aina nyingine ya dawa za kulevya kwa watumiaji. Baadhi ya madhara hayo ni kama ifuatavyo:

### Kiafya

Dawa hizi husababisha magonjwa ya akili kwa haraka, kupungua kwa uwezo wa kufikiri, kupoteza kumbukumbu. Zinaweza kusababisha madhara makubwa ya mfumo wa fahamu na hata kifo kwa matumizi ya muda mfupi. Aidha, matibabu ya uraibu wa dawa za kulevya za NPS *(New Psychoactive Substances)* si rahisi kwa sababu dawa hizi ni za kemikali na hubadilika mara kwa mara, hivyo kufanya utafiti kuwa mdogo kuhusu athari zake na njia bora za matibabu. Zaidi, hakuna dawa maalum za kutibu uraibu wa NPS kama ilivyo kwa uraibu wa dawa za kulevya kama vile heroin.



## Kijamii

Matumizi ya NPS huathiri uwezo wa mtu kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii na kiuchumi, kwani watumiaji wengi hupoteza nguvu kazi na kushindwa kujitegemea kifedha. Hali hii huongeza mzigo kwa familia na jamii kwa kuwa wanategemea wengine kwa msaada wa kifedha na kijamii na kupoteza nguvu kazi muhimu katika ustawi wa taifa.

## Kisaikolojia

Matumizi ya dawa hizi husababisha utegemezi na uraibu wa hali ya juu, ambapo mtumiaji hupoteza uwezo wa kujidhibiti na hatimaye huweza kujidhuru au hata kupoteza maisha kutokana na kuzidisha kiwango (overdose).

## Kiuchumi

Familia na serikali hulazimika kutumia gharama kubwa kwa ajili ya huduma za matibabu ya waathirika wa dawa hizi. Aidha, vijana wanaoathirika hushindwa kufanya kazi au kujitegemea, hivyo kuongeza hali ya umaskini kwa familia na taifa kwa ujumla.

## Wajibu wa jamii katika kuwalinda vijana dhidi ya tishio la matumizi ya dawa mpya za kulevya

Jamii ina jukumu muhimu katika kuwakinga vijana wasijihusishe na matumizi ya dawa za kulevya kwa sababu ni nguzo ya kwanza ujenzi wa maadili, mwongozo, na msaada wa kihisia kwa vijana. Hatua muhimu zinazoweza kuchukuliwa kuinusuru hali hii ni pamoja na:

**i. Kujenga Mazingira ya Upendo na Mshikamano;** Jamii inapaswa kuonyesha upendo, ushirikiano, na msaada kwa kijana ili kumfanya ajisikie salama na kuthaminiwa. Mazingira yenye

*>>> Inaendelea Ukurasa wa 8*

# Dawa Mpya za Kulevya Tishio Jipya Duniani

*<<< Inatoka Ukurasa wa 7*

amani na mawasiliano mazuri yanamzuia kijana kutafuta suluhisho la matatizo yake kupitia madawa ya kulevya.


**ii. Elimu na uhamasishaji;** Wazazi wanapaswa kuwapa vijana elimu kuhusu hatari za matumizi ya NPS, ikiwa ni pamoja na madhara yake kiafya, kisaikolojia, na kijamii.Kuwaelimisha vijana kutawasaidia kuepuka ushawishi wa rika.

**iii. Kuwa mfano mzuri;** Kwa kuwa vijana huiga tabia za watu wa karibu nao wazazi na ndugu wakubwa wanapaswa kuepuka matumizi ya vilevi na dawa haramu ili kuwaepusha vijana kuiga tabia hiyo. Kuonesha maadili mazuri na nidhamu huchochea kijana kuiga tabia chanya.

**iv. Kuweka mipaka na nidhamu;** Jamii inapaswa kuweka mipaka ya wazi kuhusu mambo yanayokubalika na yasiyokubalika, kama vile kutohusika na dawa za kulevya. Nidhamu shirikishi isiyo na mabavu, inaweza kusaidia vijana kuelewa athari za maamuzi mabaya.

**v. Kuwasiliana Mara kwa Mara;** Mawasiliano ya wazi kati ya wazazi na watoto husaidia vijana kuelezea changamoto zao na kuepuka kutafuta msaada mahali pengine, kama vile kwa marafiki wanaoshawishi matumizi ya dawa za kulevya. Jamii inapaswa kusikiliza matatizo ya kijana na kutoa suluhisho la kipekee.

**vi. Wazazi wanapaswa kufuatilia shughuli za kila siku za kijana, marafiki anaoshirikiana nao, na mitandao ya kijamii anayotumia.** Ushiriki wa karibu unasaidia kugundua mapema mabadiliko ya tabia yanayoweza kuashiria matumizi ya dawa za kulevya.



Tukisimama pamoja, tutaweza kupunguza athari za dawa hizi hatari na kusaidia vijana wetu kujenga maisha yenye mwelekeo mzuri na mafanikio kwa ustawi wa Taifa.

**vii. Vijana wanapaswa kufundishwa jinsi ya kusema "hapana" kwa shinikizo la rika linalowashawishi kutumia madawa.** Jamii inaweza kusaidia kujenga ujasiri wa kijana kupitia michezo, ushauri wa kisaikolojia, na kushiriki kwenye shughuli za kijamii chanya.

**viii. Kuwashirikisha Kwenye Shughuli za Kijamii;** Kuwashirikisha vijana kwenye shughuli za manufaa kama vile michezo, muziki, dini, na kazi za kujitolea ili kuwajengea malengo na kuwafanya wajihisi wana umuhimu.

**ix. Kugundua na Kushughulikia Mapema Ishara za Hatari;** Jamii inapaswa kuwa makini na mabadiliko ya tabia, kama vile kujitenga, mabadiliko ya kihisia, na kupungua kwa ufaulu shuleni, ambayo yanaweza kuwa ishara za matumizi ya dawa za kulevya. Ikiwa kijana anaonyesha dalili, Jamii inapaswa kutafuta msaada kutoka kwa wataalamu wa afya ya akili au mashirika yanayoshughulikia uraibu.

**x. Kuimarisha maadili ya kidini kunaweza kuwapa vijana msingi thabiti wa maadili.** Imani imara inawasaidia vijana kuepuka vishawishi vya kutumia dawa za kulevya.

Kwa pamoja, tunaweza kuwalinda vijana dhidi ya madhara ya dawa za kulevya kwa kuwapa elimu sahihi, msaada wa kijamii, na mazingira salama ya malezi. Ushirikiano wa wazazi, walimu, serikali, na jamii kwa ujumla ni nguzo muhimu katika mapambano haya. Tukisimama pamoja, tutaweza kupunguza athari za dawa hizi hatari na kusaidia vijana wetu kujenga maisha yenye mwelekeo mzuri na mafanikio kwa ustawi wa Taifa.





*PIPI za heroin*

Shuhuda

# Safari Yangu ya Kupona kutoka Uraibu wa Dawa za Kulevya



NAITWA Nadhiri, nina umri wa miaka 35. Kwa miaka kumi na tano, nilitumia dawa za kulevya, lakini sasa ninapata tiba kupitia kliniki ya MAT mjini Tanga. Namba yangu ya usajili ni MAT/452.

Nilianza kutumia dawa za kulevya nikiwa mwanafunzi wa kidato cha pili katika shule ya Uwidhini, Tanga. Nilianza kwa kuvuta sigara kutokana na ushawishi wa marafiki, kisha nikajaribu bangi. Hata hivyo, bangi haikunipa hisia nilizotamani, hivyo nikaanza kutumia pombe. Pombe nayo haikuniridhisha, hadi nilipokutana na rafiki yangu aliyekuwa anatumia heroin. Nilipojaribu nilivutiwa na ulevi wake na nilihisi kuwa heroin ndiyo dawa ya kulevya niliyokuwa naitafuta. Kuanzia hapo nilijikuta natumia heroin hadi nikamaliza shule ya sekondari.

Kadri miaka ilivyopita, uraibu wangu ulinifanya nipoteze uhusiano mzuri na jamii, familia, na watu waliokuwa karibu nami. Sikuwa mwaminifu, nilijitenga, na hata nikaanza kuwazuru watu ili nipate pesa za kununua heroin. Ilifika wakati ambapo niliamua kutafuta msaada. Nilijiunga na sober house kwa mara ya kwanza na nikakaa kwa miezi minne, lakini nilipotoka nilirudia matumizi ya dawa. Baada ya miaka mitatu, nilijaribu tena kwa kukaa *sober house* kwa miezi tisa, lakini bado nikajikuta nimerudi katika matumizi yad awa za kulevya.




Sasa nina miaka mitatu nikitumia dawa ya Methadone na namshukuru Mungu ninaendelea vizuri.

Hatimaye, nilikutana na asasi ya *Gift of Hope Foundation,* ambao walinishawishi nijiunge na kliniki ya MAT. Niliporidhia na kuanza tiba, maisha yangu yalianza kubadilika. Sasa nina miaka mitatu nikitumia dawa ya Methadone na namshukuru Mungu ninaendelea vizuri. Uhusiano wangu na jamii umeimarika, nimeoa, na sasa nina watoto wawili.

Mbali na kupona, nimeweza pia kujitegemea kiuchumi. Zamani nilitegemea familia kwa kila kitu—chakula, mavazi, na mahitaji mengine. Lakini sasa ninajitegemea na hata nimepewa nafasi kama mwelimishaji rika kupitia asas ya *Gift of Hope Foundation.* Kupitia nafasi hii, ninajitolea kuwapa elimu waraibu wengine ili nao waweze kuachana na matumizi ya dawa za kulevya.Safari ya kupona ni ngumu, lakini inawezekana. Na mimi ni ushuhuda wa hilo.




MHE. Kassim Majaliwa Ma (Mb) Waziri mkuu wa Jam ya Muungano wa Tanzania akionesha kit cha Sera ya T ya Kudhibiti Kupambana Dawa za Kul 2024 baada y kuzinduliwa Maadhimisho Kitaifa ya Si ya Kimataifa Kupiga Vita za Kulevya ji Mwanza.



MKEMIA kutoka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya akionesha namna ya upimaji wa sampuli za dawa za kulevya kwa wajumbe wa Kamati inayosimamia Kanuni na Sheria ndogondogo ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar walipofanya ziara katika maabara ya Mamlaka.



KIONGOZI wa wananchi wenye Imani ya ra akizungumza mara baada ya kundi hilo kup matumizi na biashara ya dawa za kulevya n Kupambana na Dawa za Kulevya.



WANAFUNZI wa Kanda ya Ziwa wakipewa elimu kuhusu tatizo la dawa za kulevya katika programu endelevu ya elimu shuleni inayofanywa na Mamlaka.



Maafisa wanawake wa Mamlaka wakiwa na katika kituo cha MAT Temeke katika kuadhi

*ıssim*
*ı Majaliwa*
*ziri*
*ı Jamhuri*
*gano*
*ınia*
*ı kitabu*
*ya Taifa*
*biti na*
*ına na*
*Kulevya*
*da ya*
*ıwa katika*
*ıisho ya*
*ı Siku*
*aifa ya*
*'ita awa*
*va jijini*



*KAMISHNA Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya akiwa na wadau baada ya kupata tuzo kutambua mchango wao katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.*



*va rastariani Jijini Mwanza*
*kupewa elimu juu ya athari za*
*va na Mamlaka ya Kudhibiti na*

*WAJUMBE wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria wakipata maelezo kuhusu kituo cha taarifa na huduma kwa wateja (call center) cha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na dawa za Kulevya.*






*ı na waraibu wanawake wanaopata matibabu*
*ıdhimisha Siku ya Wanawake Duniani.*



*JAHAZI lililokamatwa likiwa na shehena ya dawa za kulevya katika bahari ya Hindi.*

Mafanikio



*KILOGRAM 3,500 za dawa za kulevya aina ya methamphetamine na heroin zilizokamatwa wilaya ya Kigamboni, jijini Dar es Salaam kufuatia operesheni iliyofanywa na Mamlaka.*

# Serikali ya Awamu ya Sita Yavunja Rekodi Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya

Na Daniel Kasokola

SERIKALI ya Awamu ya Sita, kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), imefanikiwa kufanya mapinduzi makubwa katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya kwa mwaka 2024. Mafanikio haya yamejidhihirisha kupitia ukamataji wa kiasi kikubwa cha dawa za kulevya, kuzuia mianya ya uingizwaji wa dawa hizo nchini, na kuimarisha huduma za tiba kwa waraibu. Mbali na hatua hizi, Serikali pia imeendelea kuwekeza katika utoaji wa elimu kwa umma na kuimarisha ushirikiano na wadau wa ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha udhibiti endelevu wa tatizo hili.

## Ukamataji Wa Dawa Za Kulevya

Kwa mwaka 2024, jumla ya **kilogramu 2,327,983.66** za dawa za kulevya zilikamatwa. Hili ni kiasi kikubwa zaidi cha dawa za kulevya kuwahi kukamatwa katika historia ya Tanzania. Endapo dawa hizi zingefanikiwa kusambazwa, zingesababisha madhara makubwa kwa jamii na kurudisha nyuma maendeleo ya Taifa.

Bangi iliendelea kuwa dawa ya kulevya iliyokamatwa kwa wingi zaidi, ikifuatiwa na methamphetamine, heroin, na dawa tiba zenye asili ya kulevya kama fentanyl. Aidha, kwa mara ya kwanza, dawa mpya ya kulevya aina ya *3-4 methylene-Dioxy-Pyrovalerone (MDVP)* ilikamatwa nchini. Ufanisi huu umetokana na operesheni za kiintelijensia zilizotekelezwa maeneo mbalimbali, ikiwemo Bahari ya Hindi ambako dawa za kulevya zimekuwa zikiingizwa kupitia majahazi.

Katika operesheni kubwa zilizofanyika mwishoni mwa mwaka 2024, DCEA kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola, ilikamata **kilogramu 673.2 za methamphetamine na heroin.** Kati ya hizi, **kilogramu 448.3** zilizohusisha raia nane wa Pakistani zilinaswa kwenye jahazi huku **kilogramu 224.9** zikipatikana kwenye fukwe za Bahari ya Hindi mkoani Dar es Salaam.

## Elimu na uhamasishaji dhidi ya dawa za kulevya



*AFISA wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) akitoa elimu kuhusu tatizo la dawa za kulevya kwa wanafunzi wa sekondari mkoani Mbeya, ikiwa ni sehemu ya kampeni ya kujenga uelewa kwa jamii juu ya tatizo hilo.*

Katika kuhakikisha jamii inalindwa dhidi ya athari za dawa za kulevya, Serikali imeendelea kusisitiza elimu na uhamasishaji. Kwa mwaka 2024, takribani watu milioni 28 walipata elimu kuhusu madhara ya dawa za kulevya kupitia vyombo vya habari, semina, warsha, matamasha, na matukio ya kitaifa. Hii imewezesha wananchi wengi zaidi kuwa na uelewa wa kina




*VYOMBO vya ulinzi na usalama viendelee kushirikiana kupambana na janga hili la dawa za kulevya.*

kuhusu madhara ya matumizi ya dawa za kulevya na hatua wanazoweza kuchukua ili kuepukana nazo.

## Huduma za tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya

Katika juhudi za kupanua huduma kwa waraibu wa dawa za kulevya, Serikali, kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, iliongeza vituo viwili vya matibabu ya tiba ya methadone (MAT Clinics) katika mikoa ya Pwani na Tanga, hivyo kufikisha idadi ya vituo 18 nchini. Vituo hivi vimesajili waraibu 18,170, wanaopatiwa huduma za utengamao kutokana na matumizi ya heroin na baadhi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya kama Tramadol na Pethidine.

Aidha, nyumba sita mpya za upataji nafuu (sober houses) zilianzishwa, na kufanya idadi ya nyumba hizo kufikia 62, huku waraibu 17,230 wakipatiwa huduma. Kwa upande mwingine, waraibu zaidi ya 900,000 walihudumiwa katika vitengo vya afya ya akili vilivyopo kwenye hospitali za wilaya, mikoa, na rufaa za kanda.




Mafanikio haya makubwa yamewezekana kutokana na uwekezaji wa Serikali katika teknolojia za kisasa na ushirikiano wa kimataifa. Tanzania imeendelea kushirikiana na mashirika ya kimataifa kama UNODC, INCB, INTERPOL, na taasisi za ulinzi na usalama katika mataifa jirani ili kuimarisha juhudi za udhibiti wa dawa za kulevya.

Tathmini ya hali ya dawa za kulevya inaonesha kuwa heroin imepungua sana nchini, hali ambayo imewafanya baadhi ya waraibu kutumia dawa tiba zenye asili ya kulevya kama mbadala wa dawa za kulevya. Aidha, kumekuwepo na wimbi jipya la matumizi ya dawa mpya za kulevya (NPS) ili kukwepa udhibiti. Hii ni hatari sana na inahitajika nguvu ya pamoja ili kudhibiti tishio la dawa za kulevya katika jamii yetu. Kwa kushirikiana, tunaweza kuikinga na kuiokoa Tanzania dhidi ya janga hili. Ni wakati wa kila mmoja kuchukua hatua kwa kutoa taarifa za watu wanaojuhusisha na biashara ya dawa za kulevya, kuepuka matumizi, na kuwasaidia waraibu walioathirika ili kuwarejesha katika maisha ya kawaida.

Serikali kupitia Mamlaka ya Kudhibii na Kupambana a Dawa za Kulevya, itaendelea kuwa mstari wa mbele katika kupambana na biashara na matumizi ya dawa za kulevya nchini. Mkazo zaidi umewekwa katika kutumia teknolojia za kisasa kufuatilia mitandao ya usambazaji wa dawa za kulevya, kuimarisha uhamasishaji wa jamii, na kuongeza nguvu katika matibabu ya waraibu. Pamoja, tunaweza kuifanya Tanzania kuwa taifa huru dhidi ya dawa za kulevya.




*ASKARI wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji jijini Arusha baada ya kupata elimu kinga na udhibiti juu ya tatizo la dawa za kulevya.*

# DCEA Kanda: Nguzo Imara Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya Nchini

Na Daniel Kasokola

ELIMU ni silaha thabiti na ya msingi katika mapambano dhidi ya matumizi na usambazaji wa dawa za kulevya. Kupitia elimu sahihi, jamii hujengewa uelewa wa kina kuhusu madhara ya dawa hizi, mbinu za kujikinga, na hatua stahiki za kuchukua iwapo mtu atajihusisha au kuwa katika hatari ya matumizi ya dawa za kulevya.


Kupitia mikakati mbalimbali na kwa ushirikiano na wadau, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), kupitia ofisi zake za kanda, imefanikiwa kuwafikia zaidi ya watu milioni 28 kwa elimu kuhusu tatizo hili. Ofisi za kanda zimejidhihirisha kuwa nguzo muhimu ya utekelezaji wa wajibu wa Serikali katika kujenga jamii yenye maarifa ya kutosha kuhusu dawa za kulevya.

Mafanikio haya yanatokana na mbinu za utoaji elimu zinazolenga makundi maalum ya kijamii kwa kuzingatia mvuto, mahitaji, na athari zinazowakabili. Elimu hutolewa kwa njia mbalimbali kama semina, warsha, vipindi vya redio na runinga, makongamano, mitandao ya kijamii, sanaa, michezo, na maonyesho ya wazi, ikiwa na lengo la kuhakikisha kila kundi linapata maarifa yanayolingana na hali yao.

Makundi Lengwa yanayopewa elimu kwa mujibu wa muongozo wa utoaji elimu kuhusu tatizo la dawa za kulevya ni pamoja na:-

- Watoto
- Wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo
- Vijana nje ya mfumo rasmi wa elimu
- Wazazi na walezi
- Walimu
- Viongozi wa dini na kimila
- Wataalamu wa afya
- Mashirika ya kiraia

**Watoto** ni kundi muhimu linalopaswa kulindwa na jamii nzima kwa kupewa elimu kuhusu hatari za dawa za kulevya. Kupitia mbinu rafiki kama michezo, hadithi, vibonzo na michoro, wanafundishwa kutambua na kukataa vishawishi. Elimu hii huweka msingi wa maadili mema, kuwajengea ujasiri wa kusema “hapana” na uwezo wa kuchukua maamuzi sahihi tangu wakiwa katika hatua za awali za ukuaji wao.





*BAADHI ya wananchi wa Kijiji cha Nkerege - Tarime wakipata elimu juu ya athari za kilimo cha dawa za kulevya ikiwa ni sehemu ya jitihada za serikali kukabiliana na uzalishaji wa bangi katika eneo hilo.*




*WANANCHI wakipata elimu juu  dawa za kulevya katika wiki ya Sheria iliyofanyika viwanja vya Mnazimmoja jijini Dar es salaam.*

**Wanafunzi** katika shule za msingi, sekondari na vyuo, wapo katika hatua muhimu ya ukuaji wa kifikra na kijamii. Hili huwafanya kuwa katika hatari ya kushawishiwa kujiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya, hasa kwa njia zisizo za moja kwa moja kama marafiki, mitandao ya kijamii na hata shinikizo la kimasomo. Elimu kwa kundi hili hutolewa kina na ya vitendo, ikijumuisha mijadala, makongamano, filamu za kuelimisha na ushirikishwaji katika shughuli mbadala. Vilevile, elimu hii huambatana na ushauri nasaha, ili kusaidia wale walioathirika au walio katika hatari.

**Vijana,** hasa wale walioko nje ya mfumo rasmi wa elimu, ndiyo kundi lililo katika hatari kubwa zaidi ya kujiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya. Elimu kwa vijana huzingatia madhara ya dawa za kulevua kwa undani, kuwapa mbinu za kukabiliana na shinikizo la kijamii, na kuwahamasisha kushiriki katika shughuli mbadala kama michezo, sanaa, na kazi za kujitolea. Mafunzo haya yanasaidia kuimarisha uelewa, kujiamini na kuwaepusha na vishawishi vinavyoweza kuwaingiza katika janga la dawa za kulevya.

**Wazazi na walezi** wana nafasi muhimu kama walezi wa kwanza wa maadili na tabia kwa watoto na vijana. Kupitia elimu, hujengewa uwezo wa kutambua dalili za awali za matumizi ya dawa, mbinu bora za mawasiliano na watoto wao, pamoja na malezi chanya yanayojikita katika kuelewana na kuaminiana. Hili huwasaidia pia kuwa mfano bora wa kuigwa kwa kujiepusha na matumizi ya vilevi.

**Jamii kwa ujumla** huwezeshwa kushiriki kikamilifu katika kampeni za kuzuia, kutoa taarifa kwa mamlaka husika, kusaidia waathirika na kupunguza unyanyapaa dhidi ya watumiaji wa zamani.

**Walimu** hupewa elimu ya kuwa walezi wa karibu wa wanafunzi katika kutambua mabadiliko ya kitabia, kutoa msaada wa awali wa kisaikolojia, na kushirikiana na wazazi katika kufuatilia mienendo ya watoto shuleni na nyumbani.

**Viongozi wa dini na kimila** hutumika kama daraja muhimu la maadili na miongozo ya kiroho, wakitoa mafundisho yatakayosaidia waumini kuepuka matumizi ya dawa za kulevya na kuwasaidia waliokwishaathirika.

**Wataalamu wa afya** wana mchango mkubwa katika kugundua, kutibu na kusaidia waathirika wa dawa za kulevya. Hupewa mafunzo ya kitaalamu ya utambuzi, matibabu na ushauri kwa waathirika wa dawa za kulevya, wakitoa huduma kwa huruma, weledi na bila unyanyapaa. Pia, wao ni kiungo muhimu katika kutoa ushauri nasaha na kufanya rufaa kwa huduma zaidi za kitabibu na kisaikolojia.

**Mashirika ya Kijamii (CSOs/NGOs)** hushiriki kwa kiasi kikubwa katika kampeni za elimu na utetezi kwa waraibu wada za kulevya. Elimu ya kina wanayoipata huwasaidia kupanga mikakati bora, kuendesha programu endelevu za kuzuia matumizi ya dawa za kulevya, na kusaidia waathirika kupata tiba kurejea katika maisha ya kawaida. Mashirika haya pia ni daraja kati ya wananchi na mamlaka katika utekelezaji wa mikakati ya kitaifa.

Kupitia ofisi za kanda, DCEA imekuwa mhimili imara wa kuzuia uhitaji wa dawa za kulevya nchini. Utoaji wa elimu kwa njia shirikishi na jumuishi, unaozingatia mazingira halisi ya jamii, umeonesha mafanikio makubwa katika kuimarisha ulinzi wa kijamii dhidi ya janga hili. Ushirikiano wa mamlaka, familia, jamii na taasisi mbalimbali ni silaha madhubuti ya kuhakikisha ushindi wa kweli dhidi ya matumizi na usambazaji wa dawa za kulevya nchini Tanzania.

Tuzo



# Dcea Yatunukiwa Tuzo ya Uandaaji Bora wa Taarifa za Fedha kwa Mashirika ya Umma



*TUZO ya uaandaaji bora wa hesabu kwa mfumo wa kimataifa (IPSAS) katika kipengele cha Taasisi za Serikali zinazojitegemea mwaka 2022/2023 zinazoratibiwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA).*

**Na Seleman Edward**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imetunukiwa tuzo ya uandaaji bora wa taarifa za fedha kwa mwaka 2023/2024 katika kundi la Mashirika ya Umma, ikiwa ni uthibitisho wa ufanisi wake katika usimamizi wa rasilimali za umma kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uhasibu (International Financial Reporting Standards - IFRS).

Tuzo hiyo ilitolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) katika hafla iliyofanyika tarehe 29 Novemba 2024 katika Kituo cha Mikutano cha NBAA (APC), kilichopo Bunju, jijini Dar es Salaam. Akipokea tuzo hiyo kwa niaba ya Kamishna Jenerali wa DCEA, Bw. Aretas Lyimo, Kamishna Hussein Mbaga alieleza kuwa tuzo hiyo ni matokeo ya uwajibikaji wa pamoja na nidhamu ya kifedha inayozingatiwa na mamlaka hiyo.

"Tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuiwezesha DCEA kifedha na kimkakati, hali inayotuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi mkubwa," alisema Kamishna Mbaga.

Aliongeza kuwa ushindi huo ni kielelezo cha dhamira ya DCEA si tu katika kudhibiti biashara haramu ya dawa za kulevya, bali pia katika kuhakikisha uwazi, uwajibikaji na matumizi sahihi ya fedha za umma.

Kwa upande wake, Mhasibu Mkuu wa DCEA, CPA Steven Dalasia, alisema mafanikio hayo yametokana na ushirikiano thabiti ndani ya taasisi na ufuatiliaji wa karibu wa miongozo ya matumizi ya fedha kutoka Hazina.

"Tunazingatia kikamilifu maelekezo ya Hazina kuhusu matumizi ya fedha. Ushindi huu ni matokeo ya nidhamu ya kifedha, matumizi sahihi ya rasilimali, na weledi wa wataalamu wetu wa fedha," alisema.

CPA Dalasia pia aliwashukuru wanahabari kwa kuendelea kushirikiana na DCEA katika juhudi za uelimishaji wa umma kuhusu madhara ya matumizi ya dawa za kulevya, akieleza kuwa vyombo vya habari ni wadau muhimu katika kulinda afya na ustawi wa jamii.

DCEA imeendelea kujipambanua kama taasisi inayoongoza si tu katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya, bali pia katika kusimamia kwa ufanisi mkubwa mifumo ya fedha na taarifa, ikiwa ni sehemu ya dira yake ya kuwajibika kwa umma.

Tuzo hiyo ilitolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) katika hafla iliyofanyika tarehe 29 Novemba 2024 katika Kituo cha Mikutano cha NBAA (APC), kilichopo Bunju, Dar es Salaam.

Je, Wajua?

# Imani Potofu Kuhusu Dawa za Kulevya

**"Ukiwa unatumia dawa za kulevya kwa kiasi kidogo hauwezi kuathirika."**

**Ukweli:**

Matumizi ya dawa za kulevya hata kwa kiwango kidogo huweza kumuingiza mtumiaji katika utegemezi wa muda mrefu kwani mwili huanza kuzoea, na kuhitaji dozi kubwa zaidi kila mara hivyo kuishia kuwa mtegemezi wa dawa hizo.

**"Matumizi ya bangi ni salama kwa sababu ni mmea wa asili."**

**Ukweli:**

Ni kweli bangi hutokana na mmea, lakini hiyo haimaanishi kuwa haina madhara. Bangi ina kemikali inayobadilisha namna ubongo unavyofanya kazi na kumfanya mtumiaji kuona mambo tofauti na uhalisia (hallucinate). Pia, huchangia matatizo ya akili kama vile wendawazimu (schizophrenia), msongo wa mawazo, na kushindwa kufanya maamuzi sahihi. .

**"Waraibu wa dawa za kulevya hawana tena msaada na wamepotea kabisa."**

**Ukweli:**

Kwa msaada wa wataalamu, familia, na jamii, mraibu wa dawa za kulevya anaweza kupona na kuanza maisha mapya. Huduma za matibabu kwa waraibu wad awa za kulevya hutolewa katika nyumba za upataji nafuu, vituo vya MAT na vitengo vya afya ya akili katika hospitali za rufaa.

**"Matumizi ya dawa za kulevya husaidia kusahau matatizo na changamoto za maisha"**

**Ukweli:**

Matumizi ya dawa za kulevya hayawezi kutatua changamoto za maisha badala yake huaribu fikra na kupunguza uwezo wa kutatua changamoto, na mara nyingi husababisha matatizo mapya kama ugonjwa wa akili, ugomvi, au hata vifo.

**"Watu wanaotumia dawa za kulevya ni wavivu au wana mapungufu ya kimaadili."**

**Ukweli:**

Matumizi ya dawa za kulevya huathiri watu wa makundi mbalimbali bila kujali tabia, hadhi ya kijamii, au maadili yao. Wanaweza kuwa wanafunzi, wafanyakazi, wasanii, viongozi au hata wanandoa. Wengi wao hujikuta wakitumbukia kwenye matumizi kutokana na changamoto mbalimbali za maisha kama vile msongo wa mawazo, shinikizo la marafiki, kutafuta kutuliza maumivu ya kihisia, au kukosa elimu sahihi kuhusu madhara ya dawa hizo. Shirika la Afya Duniani (WHO) na wataalamu wa afya ya akili wanalitambua tatizo la utegemezi wa dawa za kulevya kama ugonjwa sugu.

**"Matumizi holela ya dawa tiba zenye asili ya kulevya siyo hatari"**

**Ukweli:**

Dawa tiba zenye asili ya kulevya kama tramadol, morphine au valium ni salama tu zendapo zitatumika kwa kuzingatia maelekezo ya daktari. Kutumia dawa hizi bila ushauri wa daktari au kuzidisha dozi huweza kumfanya mtumiaji aangukie kwenye janga la utegemezi wa dawa hizo.

**"Tatizo la dawa za kulevya liko mijini tu na haliwawahusu watu wa vijijini"**

**Ukweli:**

Dawa za kulevya zimeenea mijini na vijijini. Elimu sahihi kuhusu tatizo hili inahitajika kote, bila kujali eneo au hali ya maisha. "

**"Matumizi ya bangi huongeza nguvu ya kufanya kazi"**

**Ukweli:**


Siyo kweli kwamba matumizi ya bangi huongeza nguvu ya kufanya kazi. Tafiti za kiafya na uzoefu wa wahusika wengi zinaonesha kuwa bangi huathiri uwezo wa akili na mwili kufanya kazi kwa ufanisi. Athari za bangi kwa afya ya mwili na akili inaweza kupunguza uwezo wa mtu kufanya kazi kwa tija.

Je, Wajua?

# Ifahamu Skanka na Athari Zake

Na Lilian Matho

SKANKA au skunk ni aina ya Bangi inayotengenezwa kwa kuchanganya aina mbalimbali za bangi.Jina hili la Skunk lilitokana na Harufu yake kali inayo fanana na mnyama Kichehe ambaye kwa kiingereza anaitwa Skunk. Aina hii ya bangi iliyoanza kutengenezwa miaka ya 1970 huko Marekani, ina kiwango cha juu cha kemikali ya kulevya iitwayo Tetrahydrocannabinol (THC). Kiwango cha THC katika Skunk kinaweza kufikia asilimia 40 hadi 60 ikilinganishwa na asilimia 5 hadi 13 ya bangi ya kawaida. Skunk inaweza kutengenezwa kwa kuchanganya kitaalamu mbegu za aina mbalimbali za bangi na kuotesha bangi aina ya Skunk au kwa kusindika kitaalamu aina mbalimbali za bangi iliyovunwa na kupata Skunk.



Katika miaka ya hivi karibuni baada ya nchi mbalimbali kuruhusu uzalishaji wa bangi kwa ajili ya biashara,na kutengenezea dawa za tiba, kilimo cha bangi kimeongezeka kwa kasi katika nchi hizo. Hali hii ilisababisha uzalishaji mkubwa ambao ulizidi mahitaji ya soko na kusababisha bangi iliyozalishwa kutonunuliwa yote.

Kwa kuwa bangi minayolimwa kihalali katika nchi hizo ina kiwango kidogo cha THC, uwezekano wa kuiuza katika masoko mharamu ni mdogo. Kutokana na hali hiyo, baadhi ya wakulima wa bangi hiyo wanalazimika kutafuta mbinu mbadala za kuuza bidhaa yao iliyorundikana kwenye maghala. Njia moja inayotumika ni kuisindika kitaalamu bangi hiyo kwa kuichanganya na aina nyingine za bangi ya kienyeji ili kupata Skunk ambayo ina kiwango kikubwa cha THC. Matokeo yake, bangi hii mpya (Skunk) inavutia kundi kubwa la vijana kutokana na ukali wake unaoleta stimu kwa haraka

Skunk inayotengenezwa kusini mwa Afrika huuzwa katika nchi mbalimbali Duniani zikiwemo za Afrika, Ulaya, Asia, Uarabuni, China na hata bara la Amerika.

Sehemu ya Skunk hiyo hupitishwa hapa nchini kwa ajili ya kuiuza katika maeneo mbalimbali ya nchi na kuisafirisha kwenda nchi mbalimbali Duniani

Kutokana na kushamiri kwa biashara hiyo, Tanzania imeathirika kwa kiwango kikubwa kwani skanka imeanza kuonekana katika miji mIkubwa na maeneo mengine nchini. Operesheni mbalimbali zilizofanywa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) zimefanikiwa kubaini kiasi kikubwa cha skanka katika maeneo tofauti nchini. Kwa mara ya kwanza skanka ilikamatwa nchini mwaka 2023 ambapo jumla ya kilogramu 1,500 zilikamatwa. Ukamataji mwingine ni Pamoja na uliohusisha kilogramu 1,815 (Mbezi Luguruni na Magomeni) kilogramu 1,350.4 (kigamboni), kilogramu 150.2 (Sinza), kilogramu 687.32 (katika operesheni nchi nzima) na kilogramu 600 (mpaka wa Zambia na Tanzania). Hadi kufikia mwezi mei, 2025 jumla ya kilo…….za Skunk zilikuwa zimekamatwa hapa nchini.

Ukamataji huu unathibitisha hatari kubwa kwa jamii na hasa vijana na watoto. Hatari hiyo huongezeka zaidi kwani wafanyabiashara wa skanka wamekuwa wakibuni mbinu ya kuzitengeneza bidhaa nyingine chakula kwa kutumia Skunk kama pipi, biscut na zingine ili kurahisisha usambazaji bila kubanwa na Mamlaka za udhibiti.

## Madhara ya skanka

Madhara ya matumizi ya Skunk yanafanana na madhara ya bangi, ila kwa kuwa skunk ina kiwango kikubwa cha THC, madhara yake yanatokea kwa haraka zaidi na kwa kiwango kikubwa.

### 1. Hatari ya magonjwa ya akili (psychosis)



Skunk imehusishwa moja kwa moja na kuongezeka kwa magonjwa ya akili, ikiwa ni pamoja na:

- Kusikia sauti zisizo halisi (hallucinations)
- Wazo za paranoia (hofu kuwa unafuatiliwa au kutishiwa)
- Kuvurugika kwa fikra au saikolojia (delusions)

Tafiti zinaonesha kuwa watumiaji wa Skunk wana uwezekano **mara 5 zaidi** wa kuugua **psychosis** kuliko wasiovuta kabisa au wanaotumia bangi yenye kiwango kidogo cha THC..

### 2. Utegemezi na uraibu (addiction)



Kiwango kikubwa cha THC husababisha utegemezi kwa haraka zaidi. Skunk inasababisha watumiaji wengi kuwa na dalili za uraibu kama:

- Kutoacha matumizi japo wanataka
- Dalili za kujiondoa (withdrawal) kama kukosa usingizi, hasira, na msongo wa mawazo

### 3. Kuharibu kumbukumbu na uwezo wa kujifunza





Skunk hupunguza uwezo wa kumbukumbu ya muda mfupi na ubora wa kujifunza, hasa kwa vijana. Inaathiri sehemu ya ubongo inayohusika na kumbukumbu.

### 4. Kuathiri maendeleo ya ubongo (hasa kwa vijana)

Watoto na vijana wanaotumia Skunk wako kwenye hatari kubwa zaidi ya:

- Kupungua kwa IQ
- Kuvurugika kwa utulivu wa kihisia
- Kupata shida za kitabia

### 5. Shinikizo la damu na moyo



THC huongeza mapigo ya moyo na shinikizo la damu, hali inayoweza kuwa hatari kwa watu wenye matatizo ya moyo. Inaweza kusababisha mshtuko wa moyo au kiharusi (**stroke**).

# Vijana Wafundwa Kuhusu Tatizo la Dawa Za Kulevya




*WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima akiwa meza kuu katika Kongamano la Vijana lililofanyika katika Ukumbi wa Mabeyo, Dodoma, ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Siku ya Kupiga Vita Matumizi na Biashara ya Dawa za Kulevya Duniani, Juni 2025.*

Na Daniel Kasokola

SERIKALI imejipanga vema kupambana na tatizo la dawa za kulevya kwa kuanzisha chombo mahsusi ambacho ni Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), ambacho pamoja na majukumu mengine ina jukumu la kupunguza madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya, kuratibu na kusimamia masuala ya tiba na huduma za utengamao kwa waraibu wa dawa za kulevya Nchini ikiwemo nyumba za upataji nafuu.

Hayo yamebainishwa na Waziri wa Mandeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Mhe. Doroth Gwajima wakati la Kongamano la Vijana lililo andaliwa mahususi kwa ajili ya elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya lililofanyika ukumbi wa Mabeyo jijini Dodoma.

"Mamlaka yetu ina jukumu la kutoa elimu sahihi kwa Umma juu ya athari za biashara na matumizi ya dawa za kulevya, kuhamasisha jamii kushiriki katika mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya. Kwa hiyo tukio letu la leo linashabihiana kabisa na malengo na mikakati ya Serikali katika kuimarisha mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya. " Mhe. Gwajima

Pamoja na hayo, Mhe. Gwajima amewasihi Vijana kuwa mabalozi wazuri wa utekelezaji wa majukumu ya Serikali dhidi ya tatizo la dawa za kulevya ikiwa nia Pamoja na kutumia mitandao ya kijamii kama majukwaa ya kuelimishana, kujadiliana na kuhamasishana kuhusu madhara ya matumizi ya dawa za kulevya badala ya kuitumia kwa mambo yasiyo na tija.


Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu kazi, Vijana na wenye ulemavu Mhe. Ridhiwani Kikwete, amewakumbusha vijana wakiwa kama viongozi wa kesho na wabeba dira ya Taifa wanawajibu mkubwa wa kujilinda dhidi ya vishawishi vya dawa za kulevya.

"Chagueni marafiki mnaowajua, epukeni makundi yanye tabia hatarishi, jengeni nidhamu binafsi, tumieni muda wenu kujifunza, kujijenga kimaadili na kujitambua" Alisisitiza Mhe. Kikwete.

Kwa upande wake Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Aretas Lyimo amewaasa vijana kuachana na matumizi ya dawa za kulevya kwani yanazima ndoto na yanaweza kuwaingiza kwenye matokeo mabaya, ikiwa ni pamoja na uraibu, vitendo vya ukatili, matatizo ya kiafya kama vile UKIMWI, magonjwa ya akili, kifua kikuu pamoja na homa ya ini.

Kongamano hili sehemu ya Maadhimisho ya Kimataifa ya Siku ya Kupiga Vita Matumizi na Biashara ya Dawa za Kulevya Duniani ambayo kwa mwaka 2025 maadhimisho haya yamefanyika jijini Dodoma.


## Katuni/Fumbo







**CHEMSHA BONGO** — **JAZA VIFUNGU VYA MANENO KATIKA VIDUARA VILIVYO WAZI:**



herufi 3
TUI, PIA, ONA, AYA, ZUA, UPO, TAA
herufi 4
TIPA, CHAI, TISA, SABA, KOMA, OMBA, AMUA
herufi 5
ALAMA, SWALI, SHIMO, CHORA, TOLEO, WANGA, SHOKA, MAMBO, FRIJI
herufi 6
KATIBA, SIMAMA, ABIRIA
herufi 8
MATATIZO, TIRIRIKA



## Katuni Mix


DOKTA, SIONI WALA SISIKII VIZURI, MUDA WOTE NAONA KAMA NAKIMBIZWA, NISAIDIE MATIBABU!
ACHA BANGI UTAPONA
UNAHUKUMIWA JELA MWAKA MMOJA KWA KOSA LA KUIBA KUKU, UNA LA KUJITETEA?
HAKIMU NISAMEHE, ILIKUWA BANGI SIYO MIMIIIIIII!
UKITAKA NILEWE HARAKA, NINUNULIE NA SKANKA!
ACHA KUNIHUSISHA NA JELA

## Katuni Story



SCAN ME

DIRA YETU: **Tanzania isiyojihusisha na biashara na matumizi ya dawa za kulevya.**

DHIMA YETU: **Kudhibiti na kupambana na biashara na matumizi ya dawa za kulevya kupitia mikakati ya kisekta kwa ajili ya ustawi wa taifa.**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana
na Dawa za Kulevya
S.L.P 80327
Dar es Salaam

8 Barabara ya Kivukoni,
11486 Dar es Salaam

**Simu:** +255 22 211 3754/57
**Nukushi:** +255 22 211 3752
**Barua pepe:** cg@dcea.go.tz
info@dcea.go.tz

***Namba ya Mawasiliano Bila Malipo (Call Centre) 119***

@dceatanzania
@dceatanzania
@dcea tanzania
DCEATV
www.dcea.go.tz